

## TUKIPENDA WENZETU

Traditional melodies

Tu - ki - pe - nda we - nze - tu ka - ti ye - tu Mu - ngu yu - po.

1. A - li - ye - tu - fa - nya tu - we ndu - gu ndi - ye Ye - su ndu - gu ye - tu.

1. chu - ki yo - te na ha - si - ra ka - ti ye - tu zi - o - ndo - ke.

2. Tukimpenda Mungu wetu kweli, tuanzie na nduguze.  
Audhiye mmoja wao, mapendoye si ya kweli.

3. Tuwe moyo mmoja, roho moja, tuwe pia kundi moja.  
Tupendane kama vile Yesu alivyotupenda.

4. Furahini nyote binadamu, mwimbieni Mungu wetu.  
Amri yake ni nyepesi, neno lake kupendana.

5. Kati ya ugomvi na fitina, na katika kisirani.  
Mungu wetu hapapendi, Mungu wetu wa amani.

6. Yesu, kiongozi wetu mwema, amri yako twajua.  
Washa nyoyo za wakristu, wapendane siku zote.